# Jarida la UQAB


Toleo 12
Januari 2018 Miladi
Rabi-ul-thani 1439 Hijriya



**Tangazo la Trump Huku Watawala Wakikosa Kuchukua Hatua Yoyote Mbele Yake**

**Maandamano Baridi Dhidi ya Kitendo cha Kisafihi cha Raisi wa Amerika Juu ya Kadhia ya Al-Quds**

**Umma Uko Tayari kwa Khilafah**

**Umuhimu wa Kuyakumbuka Mauti**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi -Halaqa 8**

**SWALI / JAWABU: Ni Yapi Yanayo Endelea Nchini Saudi Arabia?**





## VYOMBO VYA DOLA TANZANIA VYAWATIA NGUVUNI KWA UONEVU NA DHULMA WANACHAMA WATATU WA HIZB UT-TAHRIR

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 02 / 1439 Hijria | Ijumanne, 10 Rabiul-Awwal 1439 Hijria | 28/11/2017 Miladi

# Vyombo vya Dola Tanzania vyawatia Nguvuni Kwa Uonevu na Dhulma Wanachama Watatu wa Hizb Ut-Tahrir

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Hizb ut-Tahrir Tanzania inalaani vikali kitendo cha dhulma na uonevu kilichotendwa na vyombo vya dola kuwatia nguvuni wanachama wake watatu, kuwashikilia kisiri bila ya maelezo au mashauri ya wakili zaidi ya mwezi kinyume cha sheria kisha kuwabambikizia kesi za hatari na uwongo ati 'kula njama kwa ajili ya ugaidi' na 'kutekeleza kitendo cha kigaidi'. Mashtaka haya maovu kabisa ya uzushi na yasiyokuwa na kichwa wala miguu!

Wanachama waliotiwa nguvuni ni Waziri Suleiman Mkaliaganda (31) mwalimu wa sekondari aliyenyakuliwa tangu tarehe 21/10/2017 nje ya msikiti wa karibu na nyumbani kwake, eneo la Mtwara mjini, kusini mwa Tanzania, kisha kufuatia na wengine wawili Omar Salum Bumbo (49), fundi mwashi aliyenyakuliwa na maafisa wa usalama tangu tarehe 27/10/2017 kisha akafuatia Ustadh Ramadhan Athuman/Ustadh Moshi (37), mwalimu wa dini na mfanyabiashara aliyenyakuliwa mnamo tarehe 30/10/2017 nyumbani kwake. Matukio ya wawili (Umar Salum na Ustadh Moshi) yalitendeka jijini Dar es Salaam.

Omar Salum Bumbo alinyakuliwa na maafisa wa usalama, baada ya mmoja wa maafisa hao kwa ujanja kumuahidi Omar wakutane eneo fulani kana kwamba angetaka kumpatia kazi ya ujenzi. Baada ya Omar kufika eneo waliloahidiana kukutana, alitekwa nyara kwa mabavu na maafisa hao, kumsweka garini, kisha kutoweka nae, huku wakimtisha dereva wa boda boda aliyemfikisha eneo hilo kuondoka mara moja.

Amma Ustadh Ramadhan Moshi, licha ya kunyakuliwa nyumbani kwake mbele ya familia yake na kushuhudishwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa wa Magomeni Makuti 'A' kisha maafisa wa usalama waliomkamata kuahidi kwamba taarifa zake zingepatikana katika kituo cha Polisi cha karibu. Kwa masikitiko makubwa wote wawili (Omar Salum na Ust. Ramadhan Moshi) zilipita wiki kadhaa bila ya taarifa za mahala walipo wala kujua mashtaka yao, licha ya jitihada kubwa ya familia na ndugu waliokuwa na wasiwasi mkubwa kuhusu hali ya watu wao kufuatilia katika vituo mbalimbali vya Polisi. Kwa kipindi chote hiki walinyimwa haki zao msingi ikiwemo fursa ya uwakilishi wa kisheria (wakili).

Kufuatia qadhia hiyo, sisi Hizb ut-Tahrir Tanzania tunaanza kwa kuuliza, nani asiyejua dunia nzima kwamba tangu Hizb ut-Tahrir ilipoasisiwa imekuwa ikishikamana na njia safi na wazi ya ulinganizi wa mabadiliko ndani ya jamii kutoka kwa Mtume Muhammad SAAW, njia ambayo imefungika kwa kutumia upande wa kifikra na kisiasa tu bila ya kuhusisha utumiaji wa silaha, nguvu wala mabavu hata kwa siku moja? Njia isiyobadilika ambayo wanachama na wafuasi wote wa Hizb ut-Tahrir dunia nzima huwa ni sharti msingi kuiamini na kujifunga nayo na imefafanuliwa kwa kina katika vitabu na machapisho yake mbalimbali ambayo tunaomba jamii kusoma katika mitandao yetu ya kijamii iliyosambaa na maarufu ulimwengu kote.

Kisha tunauliza tena, jee vyombo vya usalama vilivyowatia nguvuni ndugu zetu, katika uchunguzi wao walipata fursa ya kupitia taarifa ya maelezo yetu yenye kufafanua malengo, njia na mwelekeo wa Hizb ut-Tahrir ndani ya Tanzania na ulimwengu mzima tuliyoyatoa kwa upana kupitia taarifa yetu kwa vyombo vya habari mara tu baada ya kongamano letu kubwa la wazi la kimataifa lililofanyika tarehe 19 Julai 2009 Msikiti wa Kichangani, jijini Dar es Salaam, na pia wanatambua kuwa sisi tumekuwa tukifanya kazi ya kulingania Uislamu kwa miaka mingi sana kwa uwazi katika jamii bila ya kujificha?

Tunaomba tena jamii kusoma taarifa yetu hiyo hapa :

http://www.hizb-ut-tahrir.info/…/press-rele…/kenyaa/392.html

Tena tunazidi kuuliza, jee vyombo vya usalama vinaelewa kwamba Hizb ut-Tahrir inafanya kazi ya kulingania Uislamu wazi kwa njia ya kifikra ulimwenguni kote zikiwemo nchi vinara wa kupambana na 'ugaidi' kama Marekani,

Endelea Uk..3

Uingereza nk. Licha ya Hizb ut-Tahrir kufanya kazi ndani ya nchi hizo wazi wazi, hazijawahi nchi hizo hata siku moja kuinasibisha na kuihusisha Hizb ut-Tahrir na vitendo vya ugaidi ? Hivi Tanzania ina miundombinu imara na thabiti zaidi ya ulinzi, usalama, ujasusi na intelegensia kuliko nchi hizo kiasi cha kudiriki kuzua uwongo usiokuwa na kichwa wala miguu kwamba wanachama hao watatu wa Hizb ut-Tahrir wameshirikiana katika kitendo cha kigaidi?

Ikiwa huo unaoitwa uchunguzi haukuyazingatia hayo tuliyotangulia kuyataja, basi utakuwa uchunguzi wa aina gani kama si uonevu na dhulma zisizokuwa na msingi dhidi ya Uislamu, Waislamu na dhidi ya hao wanachama wetu watatu ambao ni maarufu kwa usafi wao ndani ya jamii kwa kujitenga kwao mbali na kila matendo ya vurugu, uhuni, uovu na ugaidi?

Hizb ut-Tahrir Tanzania tumeshasema mara nyingi na tunaendelea kupaza sauti yetu bila ya khofu wala kutafuna maneno kwamba Sheria ya Ugaidi ni sheria ya kibaguzi iliyolazimishwa na madola makubwa ikitumika kudhulumu,kueneza khofu, kutesa, kupoteza na kuulia jamii ya Waislamu ikiwemo pia kuwanyima haki yao msingi ya kutekeleza na kutangaza dini yao ipasavyo. Na kutiwa nguvuni wanachama wetu ambao hawana hata tembe ya kutenda wala kuamini matendo ya utumiaji nguvu na mabavu katika kulingania Uislamu, ni moja katika mifano mingi ya dhulma zinazowasibu Waislamu kutokana na sheria hii kandamizi.

Kwa kumalizia, Hizb ut-Tahrir Tanzania inatoa mwito (demand) kufutwa kwa mashtaka na kuachiwa huru mara moja wanachama wake bila ya masharti, kwa kuwa hawana makosa. Aidha, tunaomba viongozi wa jamii, wanafikira, waandishi wa habari na jamii kwa ujumla kushirikiana nasi kikamilifu katika kutangaza tukio hili na kushiriki katika kampeni ya kuachiwa huru ndugu zetu kutokana na dhulma na maonevu. Hapana shaka kila mtu makini anaelewa fika kwamba kuendelea kutumika kwa sheria hiyo kukandamizia Waislamu, sheria inayotukumbusha machungu ya zama za wakoloni mabeberu ni jambo linalotuburuza kuelekea mustakbali wa hatari, sio tu kwa Waislamu bali kwa ustawi wa uadilifu kwa jamii jumla

**Afisi ya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Tanzania**



# Tangazo la Trump Huku Watawala Wakikosa Kuchukua Hatua Yoyote Mbele Yake Ni Kofi Zito Migongoni Mwao Pia Amewavua Sitara iliyo wafinika Uchi Wao!

Usiku wa leo tarehe 6-7/12/2017 Trump ametangaza Al-Quds (Jerusalem) kuwa mji mkuu wa dola ya Kiyahudi: "Katika barua kutoka ikulu ya White House mnamo Jumatano, raisi wa Amerika Donald Trump aliitambua Jerusalem kama mji mkuu wa "Israel" na kuamuru Wizara ya Kigeni ya Amerika kufanya matayarisho ya kuhamisha ubalozi wake kutoka mji wa Tel Aviv mpaka Jerusalem, na kuanza kandarasi na wajenzi… Trump akaongezea: "Huku maraisi waliotangulia wakiifanya hii kuwa ahadi kuu ya kila uchaguzi, wameshindwa kuitimiza. Leo, mimi naitimiza…" (al-Arabiya.net 6/12/2017) cha kustaajabisha zaidi, kabla ya tangazo hili, watawala wengi katika biladi za Kiislamu, waliokuwa wakitoa vitisho juu ya Al-Quds na Msikiti wa al-Aqsa, mfano wa Salman, Abbas, Abdullah, as-Sisi, na (Muhammad) VI, walijulishwa na Trump kuwa atatangaza utambuzi wake huu katika hotuba yake baada ya masaa kadhaa… ilhali wote hawa,walibakia kimya cha mtungi mithili ya wafu kuzimu, au hata zaidi ya hivyo!

Hakika, Trump katili mjinga ametekeleza, adui wa Uislamu na Waislamu; ametimiza ahadi yake kwa Mayahudi. Hakika ukafiri ni mila (dini) moja, na haishangazi kwa makafiri kusimama kwa umoja.

Lakini, cha kustaajabisha ni kuwa watawala katika biladi za Waislamu watawafuata pasi na kujali kuwa miongoni mwao. Allah (swt) asema,

(يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ)

"Enyi mulio amini! Musiwafanye Mayahudi na Manasara kuwa vipenzi. Wao ni vipenzi wao kwa wao. Na yeyote atakaye wafanya vipenzi miongoni mwenu, basi huyo ni katika wao. Hakika Allah hawaongoi watu madhalimu" [Al-Ma'ida: 51]

**Enyi Waislamu:**

Amerika iliitambua dola ya Kiyahudi tangu mnamo 1948 na kuiunga mkono baada ya hapo, watawala hawa wakanyamazia kimya, na hata kujenga urafiki na Amerika! Walifedheheshwa na kugubikwa na udhalilifu.

Dola hii ya Kiyahudi iliendelea na uvamizi wake wa Palestina yote na Al-Quds yote iliyosalia mnamo 1967, kwa uvamizi huu waliungwa mkono vilevile na Amerika, huku watawala hawa wakinyamazia kimya, na hata kuichukulia Amerika kama rafiki muaminifu na kuifanya mpatanishi wa suluhu na serikali ya Kiyahudi. Walifedheheshwa na kugubikwa na udhalilifu.

Walikuwa wanapotosha na kuhadaa kuwa Amerika ingeishinikiza dola ya Kiyahudi kuwapatia kitu ili kuasisi dola kwacho, hata kama itanyimwa nguvu za kijeshi, na Jerusalem Mashariki ingekuwa mji mkuu wake… Hivyo basi walidunishwa kwa udanganyifu huu. Hakika, hawakumuhadaa yeyote ila nafsi zao, kwa kukosa macho ya kuona mbele… Walifedheheshwa na kugubikwa na udhalilifu.

Na sasa Amerika, kwa ulimi wa Trump inatangaza utambuzi wake kuwa Jerusalem, ambayo ni ardhi ya Isra na Mi'raj, Qibla cha kwanza cha Waislamu, na ambako msikiti wa tatu kati ya misikiti mitatu ambayo Muislamu hufunga safari kuizuru, inatangazwa mashariki yake na magharibi yake kuwa mji mkuu wa serikali ya Kiyahudi… Trump aliwasiliana na watawala hawa kabla ya tangazo hili pasi na kuupa uzito wala kuutilia maanani usemi wao tasa kuwa wanaithamini Jerusalem. Aliwapigia simu kabla ya tangazo lake, na kuongezea katika fedheha na idhlali, katika hotuba ya utambuzi wake alitangaza kuwa atamtuma makamu wa raisi kwenda kubadilishana tabasamu na watawala hao. "Trump ametangaza kuwa makamu wake wa raisi, Mike Pence, atawasili eneo la Mashariki ya Kati siku zijazo,,," (alarabiya.net 6/12/2017). Na kwa hivyo ni kweli ule msemo usemao kuwa: "Yeyote ambaye ni rahisi kumdhalilisha… jeraha litakuwa na uchungu gani ikiwa uchungu wenyewe umekufa."

Enyi Waislamu: Je, wapo watu wawili wenye akili timamu watakao hitilafiana juu ya vipi kuiokoa Palestina kutoka katika makucha ya magengi ya Kiyahudi? Je, wapo watu wawili wenye akili timamu watakao hitilafiana juu ya vipi kupambana na Amerika na wengine mfano wake, nchi zinazounga Mayahudi? Je uokovu wa Palestina haupo katika kuharakisha majeshi kupigana na serikali hiyo na kuivunja mgongo wake kwa mikono yenu, kwani Allah (swt) asema,

(قَاتِلُوهُمْ يُعَذِّبْهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ)

"Piganeni nao, Allah atawaadhibu kwa mikono yenu, na awafedhehi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini" [At-Tawba: 14]

Je, uokovu wa Palestina haupo katika kutabanni hali halisi ya kivita na dola zinazounga mkono serikali ya Kiyahudi? Je, si katika maamrisho ya Allah, Ta'ala, Wenye hekima, kuwafurusha wavamizi katika ardhi ya Kiislamu waliowafurusha watu wake?

(وَأَخْرِجُوهُمْ مِنْ حَيْثُ أَخْرَجُوكُمْ)

"...na muwatoe popote walipo kutoeni" [Al-Baqara: 191].

*Endelea Uk..5*

Je, hii si amri ya Allah dhidi ya nchi zinazounga mkono Mayahudi walioivamia ardhi ya Kiislamu na kuwafurusha watu wake?

(إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَى إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ)
“Hakika Allah anawakataza kuwafanya vipenzi wale wanaowapiga vita katika dini, na wakakawatoa katika majumba yenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na anaye wafanya hao kuwa vipenzi basi hao ndio madhalimu” [Al-Mumtahina: 9]

Je, huu sio ukweli unaohisiwa na kila mwenye moyo au mwenye kusikia na kuona?

**Enyi Waislamu, Enyi Majeshi katika biladi za Waislamu:** Kimya cha watawala hawa juu ya uvamizi wa Kiyahudi kwa sehemu kubwa ya Palestina mnamo 1948 na kutoharakisha majeshi kuikomboa Palestina yote kutoka katika makucha ya Mayahudi, ni kosa kubwa na ovu zaidi… Na kufeli kuifanya hali halisi ya kivita dhidi ya nchi zinazounga mkono serikali hii ya Kiyahudi ni uhalifu vilevile… Urafiki na utiifu kwa nchi hizo ni khiana kwa Allah na Mtume wake na Waumini.

Trump amewafichua watawala hawa; amewapokonya sitara ya mwisho iliyokuwa ikiwafinika uchi wao kwa kimya chao juu ya hotuba yake ovu. Sasa vipi basi mamlaka ya biladi za Waislamu yatabakia mikononi mwao? Ni jukumu la wanajeshi kuharakisha na kuwang’oa watawala hawa wazembe (Ruwaybidha) kwa miguu yao ikiwa hawatapigana dhidi ya maadui wavamizi wa ardhi hii tukufu na hawatatabanni hali halisi ya kivita dhidi ya zile nchi zinazounga mkono serikali hiyo… Kipaumbele cha Waislamu kinapaswa kuwa kuwapindua watawala hawa na kuasisi dola ya Kiislamu: Khilafah Rashidah. Hivyo basi makafiri wakoloni hawatasubutu tena kutia mguu wao katika sehemu yoyote ya ardhi za Waislamu wala kuwadhuru, wacha serikali hii katili ya Kiyahudi ambayo imepigwa na idhlali na fedheha, kwani Allah (swt) asema,

(وَإِنْ يُقَاتِلُوكُمْ يُوَلُّوكُمُ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُنْصَرُونَ)
“Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na kisha hawatanusuriwa” [Al-i-Imran: 111].

**Enyi Waislamu, Enyi Majeshi katika biladi za Waislamu:**

Hizb ut Tahrir, kiongozi muadilifu asiye wadanganya watu wake inawaonya kutonyamaza kimya juu ya uhalifu wa watawala hawa na khiana zao, na inawaonya kutohadaiwa na upotofu wao na urongo wao baada ya siku hii. Na jueni kwamba matokeo ya kimya hiki hayatakoma tu kwa Palestina bali mbele zaidi ya Palestina.

Hakuna udhuru uliobakia, au hata mithili ya udhuru kwa wale wenye kutii amri za watawala hawa makhaini duni thamani, wanaowazuia kuiondoa serikali ya Kiyahudi na kuiregesha Ardhi Takatifu katika boma la Uislamu. Utiifu kwao katika hali hii utawaletea fedheha hapa duniani na adhabu kali kesho Akhera. Na wala hakutawanufaisha kusema baadhi ya wenzenu kuwa walikuwa tu wakiwatii waheshimiwa wao, kwani matokeo ya maneno hayo yaliyopotoka yatakuwa ni matokeo maovu pekee, kwani Allah (swt) asema,

(وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلَا)
“Na watasema: Mola wetu! Hakika sisi tuliwatii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio walio tupoteza njia” [Al-Ahzab: 67].

Hakika, kuwatii watawala hawa wajinga kunapelekea kwenye upotofu na fedheha hapa duniani na mateso uchungu kesho Akhera. Hawa ni watawala waliojitolea katika urongo, khiana, upotevu na upotofu. Kutoka kwa Jabir ibn ‘Abdallah, Mtume (saw) alimwambia Ka’ab ibn ‘Ujrah,

«أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم قَالَ لِكَعْبِ بْنِ عُجْرَةَ: أَعَاذَكَ اللَّهُ مِنْ إِمَارَةِ السُّفَهَاءِ. قَالَ: وَمَا إِمَارَةُ السُّفَهَاءِ؟ قَالَ: أُمَرَاءُ يَكُونُونَ بَعْدِي لَا يَقْتَدُونَ بِهَدْيِي وَلَا يَسْتَنُّونَ بِسُنَّتِي، فَمَنْ صَدَّقَهُمْ بِكَذِبِهِمْ وَأَعَانَهُمْ عَلَى ظُلْمِهِمْ فَأُولَئِكَ لَيْسُوا مِنِّي وَلَسْتُ مِنْهُمْ وَلَا يَرِدُوا عَلَيَّ حَوْضِي، وَمَنْ لَمْ يُصَدِّقْهُمْ بِكَذِبِهِمْ وَلَمْ يُعِنْهُمْ عَلَى ظُلْمِهِمْ فَأُولَئِكَ مِنِّي وَأَنَا مِنْهُمْ وَسَيَرِدُوا عَلَيَّ حَوْضِي»
“Hakika Mtume (saw) alimwambia Ka’b bin ‘Ujrah: “Namuomba Allah akulinde kutokana na utawala wa mazuzu (Sufahaa).” Akauliza: na ni upi utawala wa mazuzu? Akasema: ni watawala watakaokuja baada yangu wasiofuata uongofu wangu wala Sunnah zangu, yeyote atakaye wasadikisha urongo wao na kuwasaidia katika dhulma zao basi hao si katika mimi wala mimi si katika hao, wala hatakakunywa katika birika langu peponi. Na yeyote ambaye hatawasadikisha urongo wao na hatawasaidia katika dhulma zao basi hao ni katika mimi na mimi ni katika hao na watakunywa katika birika langu peponi.” (Ahmad)

Hivyo basi, Enyi Waislamu fanyeni bidi katika kung’oa utawala wao, na kusimamisha utawala wa Uislamu, mutapata ushindi wa maisha yote mawili, maisha haya ya duniani na maisha ya kesho Akhera, kwani Allah (swt) asema,

(وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ)
“Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusra ya Allah, humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu. ” [Ar-Rum: 4-5]

**Toleo kutoka kwa Ameer wa Hizb ut Tahrir**
**Sheikh Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 03 / 1439 AH | Jumamosi, 28 Rabi' al-awwal 1439 H | 16/12/2017 M


# Maandamano Baridi Dhidi ya Kitendo cha Kisafihi cha Raisi wa Amerika Juu ya Kadhia ya Al-Quds (Jerusalem)

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Mnamo Ijumaa 15 Disemba, 2017 Hizb ut Tahrir Kenya iliongoza Umma katika miji mbali mbali mikubwa katika maandamano baridi dhidi ya tangazo la hivi majuzi la Raisi wa Amerika Donald J Trump mnamo 6 Disemba 2017. **Kuwa Al-Quds (Jerusalem) sasa ndio mji mkuu wa dola ya Kiyahudi na kuamuru Wizara ya Kigeni kuandaa uhamishaji wa ubalozi wa Amerika kutoka mji wa Tel Aviv kwenda Jerusalem, na kuanza kwa kandarasi na wajenzi.**

Maandamano haya baridi yalifanywa pindi baada ya swala za Ijumaa katika misikiti tofauti tofauti katika jiji la mwambao wa pwani la Mombasa na Kwale kushutumu vikali kitendo hicho cha kisafihi na hatari cha serikali ya Amerika kilicho dhamiria kuongeza msumari wa moto juu ya vidonda vya mateso ambayo tayari yanausibu Umma kwa kupitia mikono ile ile miovu ya dola ya kirasilimali iliyo na kiu ya umwagaji damu. Katika jiji kuu la Nairobi, kuligawanywa toleo kwa waumini wa Kiislamu katika msikiti wa Jamia. Toleo hilo ambalo asili lilitolewa na Amiri wa kiulimwengu wa Hizb ut Tahrir lilikuwa na anwani:

**Tangazo la Trump Huku Watawala Wakikosa Kuchukua Hatua Yoyote Mbele Yake ni Kofi Zito Migongoni Mwao**
**Amewavua Hata Sitara iliyo Wafinika Uchi Wao!**

**Hizb ut Tahrir Kenya ingependa kukariri yafuatayo:**

Kwanza, Al-Quds ni Qiblah cha kwanza cha Umma wa Kiislamu kwa hivyo ni katika sehemu ya itikadi ya Kiislamu. Hivyo basi, sio tu ni eneo takatifu bali pia ni alama ya umoja wa Umma wa Kiislamu ulimwenguni; na ndio utakao kuwa mji mkuu wa Khilafah Rashidah kama ilivyo ahidiwa na Mtume (saw). Kwa hivyo, itabakia chini ya himaya ya Umma wa Kiislamu licha ya njama na mipango kutoka kwa Wamagharibi wakiongozwa na dola kuu duniani leo (Amerika) na washirika wake.

Pili, hali hii ya Al-Quds imetokana na tukio chungu la kuvunjwa kwa ngao ya Waislamu Khilafah kwa mikono miovu ya iliyokuwa dola kuu duniani wakati huo (Uingereza) ambayo baada ya kufanikiwa katika kitendo chao hicho kiovu ilisonga mbele na kukaribisha tangazo la Balfour na kutoa fursa ya uundaji serikali ovu zaidi duniani ya 'Israel'. Hili lilifanikishwa kwa usaidizi wa watawala vibaraka wa kiarabu ambao wamo katika ratiba ya mishahara ya Wamagharibi kutoka hapo na mpaka sasa!

Tatu, Al-Quds inalingania ukombozi wake wa haraka; na hili linaweza kufanywa pekee kupitia kuwaunganisha watoto mukhlisina wa Umma huu wa Kiislamu miongoni mwa majeshi makuu ya Waislamu walio na hamu ya kumridhisha Allah (swt) na ambao wako tayari kufa kwa ajili ya kutafuta daraja ya juu ya Pepo! Watoto hawa si wengine isipokuwa wale wanaomwaga machozi kimya kimya kila mara wanapoona ardhi yao tukufu ikiharibiwa na kuchafuliwa na kijiumbile cha Kiyahudi; huku wakinyamaza wakitaraji kuwa viongozi hawa vibaraka huenda wakaamka karibuni na kuwaamuru kunyanyua hatua zao mbele lakini hili kamwe halikutokea. Watoto hawa mukhlisina sasa wameamua kujitweka majukumu wao wenyewe sio tu katika kuikomboa Al-Quds pekee bali pia kuukwamua Umma kutokana na minyororo ya mfumo batili wa kirasilimali na itikadi yake ya kisekula ambayo ndiyo shina la hali mbaya inayoukumba Umma wa Kiislamu leo. Kwa kupitia kuzing'oa serikali za watawala hawa vibaraka na kusimamisha mahali pao serikali iliyo barikiwa ya Khilafah Rashidah kwa Njia ya Utume.


**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# "Umma Uko Tayari kwa Khilafah"



Ni wazi kwa kila muangalizi asiye na mapendeleo kuwa mvutano pekee wa kimfumo unao endelea kwa sasa katika ngazi ya kiulimwengu ni baina ya Uislamu na Urasilimali na itikadi yake ya kisekula. Mgongano baina ya Urasilimali na dola ya Ujamaa wa Kimarxi uliokuwa muungano wa Umoja wa Nchi Huru za Kisovieti (USSR) ulikuwa ni usanii na purukushani tu, kwani Ujamaa ulikuwa ni mshawasha wa haraka kwa urasilimali uliounyima muda wa kutafakari mambo kwa umakinifu, lakini pia sawia na hili ni thibitisho la kufilisika kwa akili ya mwanadamu kwa kujaribu kuchukua jukumu la Muumba katika kusimamia mambo ya waja; mikasa, maafa, majanga ya karne ya 20 ni shutma za wazi kwa akili ya kisekula katika upande wa urasilimali pamoja na upande wa ukomunisti.

Ni dhahiri kuwa mgongano huu wa hadhara hauna usawa: kwa upande mmoja majeshi ya kimagharibi yana nguvu za kijeshi za kisawa sawa, uchumi imara, na nidhamu ya kirasilimali yenye kuhisika inayotabikishwa katika mambo ya kimaisha ya kila siku katika viwango vyote, na kujihami na mtandao mkuu wa vyombo vya habari vyenye kufikia eneo kubwa na kila aina ya ushawishi katika sekta ya umma na ya kibinafsi kwa watu binafsi na jamii kwa jumla, kieneo na kilimwengu. Kwa upande mwengine, hadhara ya Kiislamu imetoweka kabisa katika hali halisi, kwa kule kujiweka mbali kwa watawala wa biladi za Kiislamu na utabikishaji wa Sharia kama mfumo kamili wa kimaisha, na badala yake kuridhia urasilimali ulio lazimishwa na Wamagharibi. Hivyo basi, swali linalojitokeza ni je, tutaelezaje kuhusu msururu wa taarifa zinazotolewa na viongozi wakuu duniani: George W Bush, Tony Blair, Nicolas Sarkozy, Vladimir Putin, Dmitry Medvedev, Charles Clarke na wengineo, ambapo wote katika hali tofauti tofauti wameapa kuzuia kuibuka kwa serikali ya Kiislamu na hivyo basi kuchukua kila hatua ya tahadhari kwa jaribio lolote la kutabikisha Sharia?? Nitamnukuu George W Bush pekee alipotangaza wazi mnamo 16 Septemba 2001 (siku 5 baada ya tukio la 9/11 ambalo kuna uwezekano mkubwa lilipangwa na vyombo vya usalama vya Amerika) **"hivi ni vita vya msalaba, vita hivi dhidi ya ugaidi vitachukua muda"**. Pia alionya kuwa "wanamgambo wanaitakidi kuwa kudhibiti nchi moja kutawajumuisha pamoja Waislamu nyuma yake, kuwawezesha kupindua serikali zote 'poa' za eneo hilo na kuasisi utawala wenye msimamo mkali utakao anza Uhispania mpaka Indonesia."

Lau kama maono ya utabikishaji Sharia ingekuwa ndoto ya mbali, basi hakuna hata mmoja kati yao angejisumbua kuipinga, na kutoa vitisho wazi wazi vya kupigana na kurudi kwake! Ahmad Tumeh, aliyekuwa kiongozi wa serikali pinzani ya Syria aliyeko mafichoni, mnamo Novemba 11, 2015 alisema, amri ya kimataifa (yaani, dola za kimagharibi) kamwe haiwezi kukubali utabikishaji wa Sharia. Kuitisha utabikishaji wa Sharia ni jambo lisilo wezekana kulingana na uamuzi wa dola za kimagharibi; akasonga mbele na kutahadharisha kuwa "matakwa haya yatamaanisha umwagikaji mkubwa wa damu kwa ajili ya kuizuia", yaani, dola za kikoloni za kimagharibi zimejitolea kidete katika kupiga vita kurudi kwa Uislamu kama mfumo kamili wa maisha.

Licha ya hayo, Waislamu wanaitakidi imani msingi ya Itikadi ya Kiislamu: **Hakuna Mola ila Allah, na Muhammad ni Mtume Wake**. Hivyo basi, viongozi wa kimagharibi, licha ya nguvu zao zote zisizo na mithili katika historia ya hivi karibuni na zamani, bado wana mapungufu ya kibinadamu; na licha ya majivuno yao wao si miungu, na nguvu zao za kijeshi haziwapi idhini ya kuzifanya sera zao za kihalifu kuwa haki, kando na kutaja vyombo vyao viovu vya habari walivyo navyo, na teknolojia ya kisasa katika kulemaza rai jumla ya kiulimwengu.

Allah Ta'ala amewawajibisha Waislamu kuishi kuambatana na mfumo wa maisha wa Kiislamu,

*Endelea Uk..8*

katika hali yoyote ile, na kufanya kazi kuurudisha ikiwa haupo; si kwa sababu ya kutaharaki dhidi ya unyanyasaji, lakini kwa sababu ni jambo la kimaumbile kwa Waumini kuishi kuambatana na muongozo wa Allah, na kuuonyesha ulimwengu mzima uzuri wa dini Yake.

Umma wa Kiislamu umekataa hatma ya mwanzoni iliyo amuliwa juu yake na miji mikuu ya mbali ya kimagharibi. Mustakbali uliobuniwa na Wamagharibi kwa karne kadhaa ili kuufanya Umma uachane na Uislamu, uvunje ngao yake ya Dola ya Khilafah na kufikiria na kufanya kama wafanyavyo wengine. Kilicho salia katika muundo wa wamagharibi juu ya Umma pia kinakwenda kikidhaifika kila uchao huku ulimwengu wa Kiislamu ukiendelea na mwamko wake kamili kutokana na majanga ya karne iliyopita.

Kuupima Umma kiwango ulichofikia kwa sasa si vigumu. Kura za maoni na tafiti kadhaa zimeonyesha hamu hiyo ya kutaka umoja, na hata ikiwa mtu atakuwa na shaka juu ya kura hizi za maoni, kuna ushahidi wa kutosha kutoka katika ulimwengu wa Kiislamu, kuwa raia wake wanawakataa Wamagharibi na vibaraka wao waziwazi na kuitisha Sharia na serikali ya Kiislamu. Lengo la uwepo wa kigeni katika ardhi za Waislamu ni kupanda mbegu ya mizozo na kugandamiza ulinganizi wa Khilafah.

Muongo mmoja na nusu uliopita umethibitisha kuwa miito ya kuzigeuza biladi za Kiislamu kwa hadhara ya kimagharibi inaambulia patupu. Hakuna yeyote aliyeshindwa kushajiishwa na ujasiri wa Waislamu wa Mashariki ya Kati. Mwaka wa 2011 ulishuhudia kufurika kwa watu mabarabarani kama njia ya kuonyesha upinzani wao nchini Tunisia, Misri, Libya, Yemen na Syria. Ingawa vibaraka wapya wamewekwa na chaguzi kufanywa: mapambano bado yanaendelea. Upinzani wa watu hawa ulilenga watawala katili, ushawishi wa kimagharibi na kimsingi dhidi ya nidhamu mbovu katika biladi zetu za Kiislamu, ambazo zimedumu katika kufeli kupeana hata mahitaji msingi kwa watu wetu.

Matukio haya pia yanatoa ushuhuda kuwa mpangilio wa sasa wa siasa za eneo, ulio shinikizwa na wakoloni wa kimagharibi kwa lengo la kuugawanya Umma, umefeli vibaya mno: nyoyo na akili za Waislamu zimeungana na kuonyesha umoja wao na huruma kwa ndugu zao Waislamu kote ulimwenguni: kuanzia Waislamu wa jamii ya Uyghur katika nchi iliyo kaliwa ya Turkestan, mpaka Rohingya, eneo la Asia ya Kati, Kashmir na Afghanistan, mpaka eneo la Afrika ya Kati, na kitovu cha maeneo yote haya kikiwa ni: Msikiti wa Aqsa na ardhi tukufu inayo uzunguka, Ash Sham kama ilivyo katika Surah Al-Isra.

Ndio dola za kimagharibi zimepanga njama zote, na kubuni kila aina ya urongo pamoja na unyama wa nchi za kiaskari zikiongozwa na vibaraka wake, walio jaribu kucheza karata za ukabila, ujamaa, demokrasia na urasilimali, ambazo zote zimefeli na hivyo basi kufungua njia kwa Waislamu kutambua kwa ukamilifu kwamba suluhisho pekee ni Uislamu.

Haishangazi kuwa Hizb ut Tahrir imeshiriki pamoja na Umma katika ya mvutano dhidi ya njama ya kimagharibi. Da'wah ya Hizb ut Tahrir imesambaa mbali na kwa mapana huku ikikumbatiwa na nyoyo na akili za waumini mukhlisina, wanaume kwa wanawake, wazee kwa vijana, eneo la Turkestan, Asia ya Kati, Indonesia, Malaysia – huku kongamano hili likiwa ni ushahidi tosha, Bangladesh, India, Pakistan, Afghanistan, katikati mwa eneo la Tatarstan, Caucasus, Crimea, vile vile Uturuki na biladi za kiarabu, huku ikifika mpaka Kenya na Nigeria. Mbegu za mwanzo za da'wah hii iliyo barikiwa zilipandwa mjini Jerusalem, na mti mkuu wa da'wah hii ukaota mizizi kwa haraka nyoyoni na akilini mwa Waislamu eneo la Sham, Misri, Libya, na Tunisia. Mti huu mzuri kwa sasa unatoa kivuli kwa Umma wa Kiislamu karibu kila mahali.

Hizb ut Tahrir imefaulu kikweli kuunganisha Waislamu katika hamasa, itikadi, fikra na fahamu zao juu ya vizingiti vyote: haijali anakotoka Muislamu (mwanamume au mwanamke): anaweza kuwa anatoka Kenya au Bengal au Uzbekistan, anaweza kuwa ni wa dhehebu la kifiqhi la Hanafi, au Shafi, au Hanbali, anaweza kuwa mweupe au Malay au mweusi… lakini umbile lake la kindani la kibinadamu yeye ni muumini kwa Allah Subhanahu wa Ta'ala, na amejitolea kwa dhati kujisalimisha katika kumuabudu Bwana wa Ulimwengu… na huu ndio uzuri wa Uislamu, kuwa ni ujumbe wa rehma kwa wanadamu wote: sio kwa Waarabu, wala kwa Wafursi, wala kwa Wakurdi, wala kwa Waturuki pekee. Uislamu unawajibisha kuwa Muislamu awe ndugu ya Muislamu mwenzake, na Uislamu uko wazi kwa yeyote atakaye kuukumbatia pasi na mapendeleo yoyote au uzushi wa watu.

Hapa ndipo penye matunda ya Hizb ut Tahrir: kwa kufaulu kuunda jukwaa la kuunganisha Umma kikweli katika mvutano wa kurudisha Uislamu kama mfumo kamili wa maisha; chini ya Sharia ya Kiislamu haijalishi ikiwa Imam/Khalifah atatabanni ijtihadi hii au ile, kwani zote zachipuza kutoka katika Itikadi ya Kiislamu na uteremsho wa wahyi ndani ya Qur'an tukufu. Zaidi ya hayo, Hizb ut Tahrir imeonyesha wazi wazi njia ya kufikia utabikishaji kamili wa Sharia katika kukabiliana na kadhia zote za kimaisha. Hizb ut Tahrir imetoa vitabu vingi vikiwemo katiba kielezo, na vitabu vinavyo fafanua kwa kina nidhamu ya kiuchumi, ya kisiasa, ya kielimu, ya kifedha, siasa za kimataifa pamoja na ubebaji ulinganizi ulimwenguni kupitia Jihad. Na hasha katu hatutaogopa kulingania Jihad kama chombo cha kulingania ujumbe wa Uislamu ulimwenguni; hatuwezi kubadilisha wala kupinda amri ya Allah Subhannahu wa Taala, aliye amrisha katika Qur'an amri ya dhahabu ya kutolazimisha katika dini. Watu wako huru kufuata ukinaifu wao: ima kwa kukubali Uislamu au kuukataa.

***Endelea Uk..9***

Mafanikio ya Hizb ut Tahrir hayako tu katika kutoa muono safi katika kurudisha Uislamu kama mfumo kamili wa maisha kupitia kutabikisha Sharia chini ya dola ya Khilafah, bali pia yako katika kuzalisha kizazi cha wabebaji ulinganizi miongoni mwa sekta kadha wa kadha za Umma, katika kila biladi ya Kiislamu. Yeyote anayefuatilia mjadala huu wa hali zilizoko kwa sasa hawezi kukosa kutambua kuwa kutakikana kwa Uislamu kama mfumo kamili wa maisha chini ya Khilafah kumetawala anga.

Orodha ndefu ya vipindi vya runinga, makala ya magazeti, fatwa (au fatwa za kirongo) zilizotolewa na mashekhe "rasmi", watumishi wa hawaa za madikteta nchini Misri, Jordan, Tunisia, Morocco, Uturuki, Tajikistan, Uzbekistan na nchi nyenginezo, orodha ni ndefu mno kiasi cha kukosekana nafasi ya kutosha hapa kuitaja yote. Ni ushahidi wazi kuwa dola za kikoloni za kimagharibi zinaogopa kuendelea kukua kwa ulinganizi wa Khilafah miongoni mwa Waislamu. Wakati Saudi Arabia ilipo amua kuasisi kituo cha kupambana na misimamo mikali kwa ushirikiano na ikulu ya White House, na kuwafuta kazi takriban maimamu 3000, na kufungua mlango kuruhusu ugeuzwaji wa jamii kwa hadhara ya kisekula ya kimagharibi chini ya kisingizio cha "burudani", yote haya pamoja na kuimarisha uhusiano na wavamizi wa Kiyahudi wa Palestina, matukio yote haya yanathibitisha kuwa ulimwengu wa Kiislamu umeungana pamoja kukabiliana na vibaraka hawa wa dola za kimagharibi.

Baadhi ya watu wamekuwa wakiikashifu Hizb ut Tahrir kwa muda mrefu kwa kuwalingania viongozi wa majeshi ya Kiislamu kutoa nusrah kusimamisha Khilafah; matukio ya hivi majuzi eneo la Mashariki ya Kati yamethibitisha uhalali wa msimamo wake: kuanzia Algeria (1991) mpaka kwa mapinduzi ya kiarabu (2010 mpaka sasa). Ni wazi kuwa matakwa thabiti ya kurudisha Uislamu kama mfumo kamili wa maisha ni sharti ya ambatanishwe na usaidizi kutoka kwa miongoni mwa majeshi, ambao ni watoto halisi wa Umma, ili kuweza kujikomboa kutoka kwa udhibiti wa kikoloni na ili Umma uweze kufurahia matunda ya Sharia, ambayo si jengine isipokuwa ni rehma kwa wanadamu wote.

Dola za kimagharibi zimeamua kuanzisha kampeni ya kuichafulia jina Hizb ut Tahrir kwa kujaribu kwa fadhaiko kuinasibisha na ugaidi, ili kuhalalisha msako wao wa kinyama dhidi ya amali zetu. Alhamdulillah ulinganizi wetu hauhitaji kuhamiwa: tumeapa kuanzia siku ya kwanza kufuata nyayo za Mtume (saw) katika ubebaji ulinganizi, na vile vile tumefafanua wazi njia yetu kuwa tunafanya kazi na Umma ili pamoja tujenge rai jumla na uaminifu kwa Uislamu kama mfumo kamili wa maisha, na wakati huo huo kufichua ukweli juu ya serikali hizi fisadi zinazotumikia maslahi ya wamagharibi; katika kutekeleza mvutano wa kifikra pamoja na mvutano wa kisiasa, Hizb ut Tahrir kamwe haijawahi kuchukua msimamo kwa msingi wa kukubaliana na hali halisi au kujaribu kulegeza misimamo. Kilicho iwezesha Hizb ut Tahrir kufuata mkondo huu wa vitendo ni kule kuwa haitafuti isipokuwa radhi za Allah Subhannahu wa Taala pekee, na, huku ikijua kikamilifu maumbile ya serikali hizi fisadi, Hizb ut Tahrir imezipinga zote na imezichukulia zisokuwa za halali machoni mwa Sharia.

Katika wakati ambapo mfumo wa kiulimwengu wa kirasilimali unaugua kutokana na mgogoro mbaya katika ngazi zake zote: kisiasa, kijamii, na kiuchumi, wakati umewadia kwa mwamko mapya ya Uislamu.

Tumesoma taarifa kadha wa kadha kutoka kwa maafisa wa kuu wa Amerika kwamba ni wakati sasa wa kuuzika mpangilio wa Sykes-Picot, na kuunda upya ramani ya eneo hili ili kutumikia maslahi ya Amerika. Lakini sisi twasema wakati umewadia sasa kwa waumini mukhlisina wa Umma huu kufanya kazi nasi kujishindia jaha ya kuurudisha tena Umma wa Kiislamu mahali pake panapo stahili: pa kuongoza wanadamu kutokana na mateso na giza la mfumo wa kisekula wa kirasilimali uliofeli na kuwapeleka katika nuru na rehma ya Uislamu. Tunawasihi nyote na kwa wale wanao tutazama kuungana na njia hii ya kuunganisha Umma huu katika kuifahamu dini hii pamoja na kuitisha kurudi kwa Uislamu kama mfumo kamili wa maisha.

Vile vile tunawasihi wanajeshi na maafisa mashujaa wa majeshi ya Kiislamu kuharakisha katika kupata radhi za Allah Subhannahu wa Taala, kwa kutoa nusrah kwa Hizb ut Tahrir, kama ilivyo jitokeza katika Surah Al-Anfal,

**﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ﴾**

"Enyi mlio amini! Muitikieni Allah na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Allah huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mutakusanywa" [Al-Anfal:24]

Namalizia kwa kuwakumbusha nyote kuwa Allah (swt) Mola wa Ulimwengu ameapa, na kiapo chake ni cha kweli, kuwa dini hii itatawala, basi tufanyeni bidii sote kujishindia jaha hii ya kuwa waja mukhlisina wa Allah wanaostahiki ushindi wake.

**﴿إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَٰئِكَ فِي الْأَذَلِّينَ * كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ﴾**

"Hakika wale wanao mpinga Allah na Mtume wake, hao ndio miongoni mwa madhalili wa mwisho. Allah ameandika: Hapana shaka mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda." [Al-Mujadalah:20-21]

**Dkt. Osman Bakhash**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**Kwa Ajili ya Kongamano la Khilafah Nchini Malaysia Mnamo 21 Rabii' I 1439 H - 9 Disemba 2017**

# Umuhimu wa Kuyakumbuka Mauti



Moja katika maudhui yanayokwepwa na Jamii ya kiliberali kimakusudi kuyazungumzia ni mauti. Hii inakuja kwa kinachotokamana na itikadi yao ya Kisekula kwamba shabaha kuu ya maisha ya wanadamu hapa duniani ni kujipatia nafasi na kiwango kikubwa cha starehe. Kwa mtazamo huu ndio watu wengi leo hukataa kuyazungumzia mauti.

Uislamu umetuelekeza jinsi ya kufahamu umauti nayo humaanisha kutoka katika maisha ya duniani na kwenda kukutana na Mwenyezi Mungu (swt). Mwenyezi Mungu (swt) anasema:

**Sema 'Hakika mauti haya mnayoyakimbia, bila shaka yatakutana nanyi, kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri hapo atakujulisheni (yote) mliyokuwa mkiyatenda.** [Al-Jumu'ah:8]

Licha ya hayo Uislamu pia ukafafanua kuwa mtu yeyote hawezi kufa ila kwa matakwa na amri ya Mwenyezi Mungu (swt). Hivyo sababu ya umauti ni moja tu nayo ni kumalizika kwa umri wa mwanadamu. Muislamu lazima aitakidi kuwa afishaye si mwengine ila ni Mwenyezi Mungu (swt) pekee.

Kukumbuka mauti maana yake ni kuikumbuka akhera yaani kufahamu mwanadamu kuwa hana budi ila iko siku atakutana na Mola wake. Aliletwa hapa duniani pasina khiyari yake basi ataondoka pia pasina mapenzi yake. Mtume (saw) ametaka Waislamu waweze kukithirisha kukumbuka mauti kama alivyopokea Tirmidhiy, An-Nasaai na Ibn Majah kutoka kwa Abu Hurairah kwamba Mtume (saw) alisema:

**'Kithirisheni katika kukumbuka chenye kuondosha ladha, yaani mauti.'**

Kuna faida nyingi mno kwa Muislamu katika kuyakumbuka mauti kila wakati lakini tutosheke na kutaja tu tano.

**Kwanza;** Humfanya Muislamu awe na haraka ya kufanya toba ya kikweli kwani hukumbuka madhambi yake na kumuomba msamaha Mwenyezi Mungu (swt) kabla ya kuondoka kwake duniani.

*Endelea Uk..11*



Email: uqab@hizb.or.ke

**Pili;** Kutosheka na kipato alichopewa na Mwenyezi Mungu (swt). Moyo kutosheka humfanya Muislamu kutokimbizana na dunia bali hushughulikia dunia huku akichunga mipaka ya Uislamu. Muislamu ana mwisho wa kuishi duniani na vilivyomo alivyoruzukiwa ataviacha na kwenda kukutana na Mola wake ambako huko ni amali njema ndiyo zinazohitajika.

**Tatu;** Huleta uchangamfu wa kufanya amali njema. Mwenye kukumbuka mauti utampata akijipinda kwa kufanya kila jema huku akijieupusha na kila ovu. Utamwona hachoki kuswali, kusoma Quran, kufanya da'wah na mengine mengi mema kwani anajua wakati wowote huenda akaondoka.

**Nne;** Muislamu anayekumbuka mauti huepukana na hasadi kwani siku zote anaonekana akiachana na mambo ya watu huku akijishughulikia zaidi yeye mwenyewe na mambo yake yatakayomfaa Akhera.

**Tano;** Huhuisha moyo wa mtu. Sababu kubwa inayopelekea moyo wa mtu kuwa hai kiasi cha kuwa walainika katika kusukuma mtu kufanya mema ni kukumbuka mauti. Amepokea Abu Hurairah kuwa Mtume (saw) alisema:

**'Fanyeni wingi wa kukumbuka mauti kwani hakuna mja yoyote ayakumbukaye kwa wingi ila Mwenyezi Mungu huhuisha moyo wa mja huyo na kumsahilishia uchungu wa mauti.'**

Kinyume cha hayo mtu asiyekumbuka mauti siku zote utamuona akiwa mvivu katika kufanya ibada, kulevywa na maisha ya dunia pamoja na kuchelewesha toba huku akizama na starehe za dunia.

Katika kukumbuka mauti kunapaswa kumsukume Muislamu ajitayarishe na mauti kwa kufanya kila aliloamrishwa na kujieupusha na kila alilokatazwa. Mtume (saw) asema:

**Mwerevu ni yule atakayedunisha nafsi yake kwa kutofuata matamanio yake kisha akafanya mema yatakayomfaa baada ya mauti, na mvivu ni yule atakayefuata matamanio ya nafsi yake huku akitamani kuwa atapewa mazuri na Mwenyezi Mungu.**

Na katika Hadithi nyengine inayosimuliwa na Ibn Umar (ra), asema:

**'Nilikuwa pamoja na Mtume (saw) mara akajiliwa na mtu miongoni mwa Answar akamsalimia kisha akamuuliza Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni Muumini yupi aliye bora zaidi? Mtume (saw) akamjibu: 'Ni yule mwenye tabia njema zaidi". Kisha akamuuliza tena: na ni nani katika Waumini aliye mwerevu zaidi akasema Mtume (saw): 'ni yule akumbukaye kwa wingi mauti na anayejitayarisha zaidi na baada ya mauti na hao ndio waerevu.'**

Mambo yafuatayo tunaweza tukayatumia kama ukumbusho wa mauti:

**-Kuzuru makaburi kila mara kwa kuwaombea waliotangulia mbele ya haki.**

**-Kumwangalia maiti akiwa amelazwa kitandani akioshwa, kukafiniwa, akiswaliwa, akiwa kwenye jeneza na hatimaye kuzikwa.**

**-Kufikiri watu wako wakaribu waliofariki dunia uliokuwa ukiamiliana nao kucheka, kupanga nao mipango ya maisha lakini walikufa huku mipango mingi yao bado ikiwa haikukamilika.**

Hivi ndivyo inatakikana Muislamu kwa hali yoyote aonekana akikumbuka tukio hili zito ambalo ni zito sana kuliko mazito yote aliyokumbana nayo maishani mwake. Akumbuke pia kuwa tukio hilo la mauti ndilo jepesi zaidi kuliko yanayofuata baada yake. Twamoumba Mwenyezi Mungu (swt) atupe mwisho mwema, aturuzuku shahada wakati wa kufa, msamaha baada ya kufa na toba kabla ya kufa. Ameen

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi Kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

# Halaqa 8: Maudhi na Adhabu kwa Mtume (saw) na Wabebaji Da'wah

Katika Halaqa hii tutazungumzia mbinu ya nne ambayo waliitumia Muqureshi dhidi ya Da'wah ya Mtume (saw) nayo ni maudhi na adhabu kwa Mtume (saw) na kwa wabebaji Da'wah.

Alivumilia Mtume (saw) shida zote na maudhi akiwa anawalingania waja kwa Allah. Maudhi yakazidi kwa Mtume (saw) na adhabu kwa wanaomuamini, na dori hii ikachukua mda mrefu. Mivutano ya kifikra na mapambano ya kisiasa yakaachukua muda mrefu takriban miaka kumi, Waislamu walipitia sampuli za adhabu.

Asema Allah (swt):

كَمَا أَخْرَجَكَ رَبُّكَ مِنْ بَيْتِكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ فَرِيقًا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ لَكَارِهُونَ

Kama Mola wako Mlezi alivyo kutoa nyumbani kwako kwa haki, na hakika kundi moja la Waumini linachukia. [Al-Anfaal 8:5]

Mtume (saw) alipata maudhi makali tofauti tofauti, ili awache Da'wah, makafiri na mushrikina walipanga njama ya kumuua Mtume (saw). Wakajaribu kumuua mara kadhaa, lakini Mtume (saw) aliendelea na subra na huku akitarajia kwa Allah. Haikudhoofika azma yake wala imani yake kwa Allah haikulainika kwa matatizo yaliyomkuba katika Da'wah, bali alibakia thabit katika mfumo, anawalingania waja kwa Allah kwa azma na thabati, ili apata Radhi za Allah, na ili awe mfano mwema na kiigizo chema kwa Maswahaba, na kwa watakaokuja baada yake mpaka kitakaposimama kiyama.

Amepokea Bukhari kutoka kwa Urwah Radhi za Allah ziwafikie asema: "Nilimuuliza Ibnul 'Aas Radhi za Allah zimfikie, nikasema: Nipe khabari jambo gani zito ambalo mushrikina walimfanyia Mtume?" Akasema: "Alipokuwa Mtume (saw) anaswali katika chumba cha Kaabah Uqbah Ibnul Muit akamwendea Mtume (saw) akaweka nguo yake katika shingo ya Mtume (saw) akamnyonga kwa nguvu, Abubakar (ra) akaja akamshika mabega yake na kumsukuma kutoka kwa Mtume (saw)."

Akasema Allah (swt):

وَقَالَ رَجُلٌ مُؤْمِنٌ مِنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَكْتُمُ إِيمَانَهُ أَتَقْتُلُونَ رَجُلًا أَنْ يَقُولَ رَبِّيَ اللَّهُ وَقَدْ جَاءَكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ مِنْ رَبِّكُمْ ۖ وَإِنْ يَكُ كَاذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهُ ۖ وَإِنْ يَكُ صَادِقًا يُصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِي يَعِدُكُمْ ۖ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ كَذَّابٌ

Na akasema mtu mmoja Muumini, aliyekuwa mmoja katika watu wa Firauni aliye ficha Imani yake: Je, Munamuuwa mtu kwa sababu anasema Mola wangu Mlezi ni Mwenyezi Mungu? Na hali naye amekujieni na hoja zilizo wazi? Na akiwa yeye ni mwongo basi uwongo wake ni juu yake mwenyewe, na akiwa mkweli yatakufikieni baadhi ya hayo anayo kuahidini. Hakika Mwenyezi Mungu hamwongoi apindukiaye mipaka, mwongo mkubwa. [Ghafir: 28]

Huu ni mfano mmoja tu wa Mtume (saw) kupata shida na maudhi kwa ajili ya daa'wah, na kuna mifano mingi inayotajwa na vitabu vya Seera haitoshi kuelezea kwa ufafanuzi hapa. Licha ya hayo, tutaitaja baadhi yake kwa ufupi sana.

Alipokufa Abu Twalib, jitu jinga moja katika wajinga wa Kikureyshi alimtupia Mtume (saw) mchanga. Mtume (saw) akarudi nyumbani, binti yake mmoja akaja na kumfuta uso wake huku akilia. Rasul (saw) akaketi na kusema: **"Ee mwanangu! Usilie, Naapa kwa Allah, Allah atamkinga babako)...!"**

Utbah Ibnu Muit alitupa juu ya kichwa cha Mtume (saw) na katika mabega yake uchafu wa ngamia akiwa Mtume (saw) amesujudu.

Abu Jahli alimkuta Mtume (saw) katika Swafaa akamuudhi mpaka Ami yake Mtume Hamzah akakasirika, akaenda msikitini akamkuta Abu Jahli akiwa katika kikao cha Maqureyshi, hakumuongelesha bali alimsimamia kichwani na kumpiga kwa uta mpaka akapasuka, wakasimama wanaume katika Maqureysh wanamzuia Hamzah: Akasema hamzah: "Dini yangu ni Dini ya Muhammad. Nashuhudia kuwa yeye ni Mtume wa Allah...!" Akasilimu papo hapo.

Mtume (saw) alipokuwa anaondoka kwa kabila la Thaqif baada ya kukosasa Nusra, watu wataifa hilo walikaa katika njia safu mbili, alipopita wakawa wanampiga mawe kila anaponyanyua mguu wake mpaka wakamtoa damu. Akapita na ilhali damu inachuruzika...!

Makafirii wa Kikureshi hawakukoma kwa mateso waliomfanyia kabla ya kusimamisha serikali, bali yalifuatia hata baada ya kusimamisha dola, siku ya vita vya Uhud waliyavunja meno yake ya mbele ya Mtume (saw) na kichwa chake kupasuliwa, akasema naye anafuta damu katika uso wake mtukufu: "Vipi watafaulu watu walioupaka damu uso wa mtume wao?!!" Akateremsha Allah (swt):

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ أَوْ يُعَذِّبَهُمْ فَإِنَّهُمْ ظَالِمُونَ

Wewe huna lako jambo katika haya - ama atawahurumia au atawaadhibu kwani wao ni madhalimu[Aal-Imran:128]

**Itaendelea katika UQAB Toleo 13…In Shaa Allah.**

# SWALI / JAWABU:
## Ni Yapi Yanayo Endelea Nchini Saudi Arabia? Amerika Inasimama Msimamo Upi Kuhusiana Nayo?



**Swali:**

Mnamo tarehe 19/11/2017, tovuti ya Al-Mudun ilifichua kuwa kampeni dhidi ya ufisadi inayoenedelea nchini Saudi Arabia imeanza kuathiri huduma ya jeshi. (Afisa wa Kisaudi, anayeifahamu vyema kampeni hii dhidi ya ufisadi nchini Saudi Arabia, alifichua kukamatwa kwa maafisa 14 wastaafu wa kijeshi waliokuwa wakifanya kazi katika Wizara ya Ulinzi, na maafisa wawili wa kitengo cha ulinzi wa kitaifa, kwa kushukiwa kuhusika katika kesi za ufisadi za kandarasi za kifedha) (Al-Mudun: 19/11/2017), na kukamatwa huku kulianza tangu tarehe 4/11/2017 ambapo Mfalme Salman bin Abdul Aziz alipounda kamati ya kupambana na ufisadi chini ya uongozi wa mfalme mtarajiwa Mohammed bin Salman, huku ikihusisha pia idadi ya mawaziri wa zamani na viongozi wa kibiashara na kusitishwa kwa akaunti zao na za jamaa zao wa karibu, (shirika la wanahabari wa kigeni (Reuters) lilinukuu – kamati ya chunguzi wa ufisadi imesitisha akaunti ya benki ya amiri Mohammed bin Nayef, mfalme mtarajiwa aliyeondoshwa mamlakani na ambaye ni mmoja wa watu maarufu zaidi katika familia tawala ya Saudi, na akaunti za jamaa zake wa karibu. Bin Nayef ndiye aliyekuwa mfalme mtarajiwa kabla ya mfalme aliyeko sasa kumbadilisha na kumueka mwanawe, Mohammad bin Salman na kisha kamati hiyo kuwakamata ma-Amiri 11…) (Shirika la habari la BBC idhaa ya Kiarabu, 8/11/2017). Ni yapi yanayo endelea nchini Saudi Arabia? Ni upi msimamo wa Amerika kuhusiana nayo?

*Endelea Uk..14*

**Jibu:**

Ili jibu lipate kueleweka kwa uwazi tutaelezea kwa mukhtasari kuhusu familia ya Saud na ushirikiano wao kisha tuendelee na jibu:

1. Familia ya Al-Saud imeshirikiana na kafiri mkoloni tangu uasi wao wa kwanza dhidi ya Dola ya Kiuthmani kama dola ya Kiislamu. Walishambulia na kutia uchochezi kwa usaidizi wa wakoloni wa Kiingereza dhidi ya Kuwait mnamo 1788, Makkah na Madina mnamo 1803-1804 na kuzivamia biladi hizi. Waliishambulia Dimishki mnamo 1810, huku wakaazi wake wakiihami kwa ujasiri mkubwa, lakini hatimaye wakaidhibiti Aleppo na miji mengine. Walipatiliza fursa ya kulitumia dhehebu la Wahhabi katika kazi yao, na Waingereza wakawatumia kuishambulia dola ya Kiislamu. Lakini baadaye, dola ya Kiislamu ilifaulu kumaliza uasi huu ulioongozwa na Al Saudi mnamo 1818, kupitia gavana wa Wilaya ya Misri, Muhammad Ali.

Walisukumwa tena na Uingereza kuanzia mwishoni mwa karne ya 19, mnamo 1891, lakini dola ya Kiuthmani ikawashinda nguvu. Uingereza ikawasukuma tena mnamo 1901, na ukuruba wao na Uingereza na usaidizi wa Uingereza kwao ukafichuka.

Waingereza walipatiliza fursa ya udhaifu wa dola ya Kiuthmani na kuingia kwake katika Vita vya Kwanza vya Dunia ili kuutia nguvu msimamo wa familia ya Saud dhidi ya watu wa Najd na Hijaz waliopigana dhidi yao vita vya muda mrefu mpaka Wasaudi walipoweza kuwashinda na kudhibiti maeneo haya na kisha kutangaza ufalme wao mnamo 1932, kwa usaidizi wa Uingereza dola iliyokuwa ikiongoza zama hizo.

Lakini baada ya Amerika kugundua mafuta nchini humo na kutokwa na mate kwa utajiri wao, walianza kutafuta ushawishi wa kisiasa nchini humo. Hili lilidhihirika kwa kuneemeka kwa watu wa familia hii ya kifalme, hususan miongoni mwa warithi wa ufalme huo watoto wa Abdul Aziz, mfalme muasisi, baada ya kifo chake mnamo 1953. Hivyo basi, mzozo kati ya Uingereza na Amerika ukaanza nchini humo.

2- Hivi sasa kibaraka wa Amerika Salman ameweza kuchukua udhibiti, na kuanza mchakato wa kuuza rasilimali za vibaraka wa Uingereza na wafuasi wao. Mtangulizi wake, aliyekuwa mfalme mwenda zake Abdallah, alihusishwa na Waingereza, na akajaribu kujishughulisha na vibaraka wa Uingereza waliokuwa mamlakani kabla ya kifo chake, lakini ada ya familia yake ya upokezaji mamlaka ilimlazimu kumteua Salman bin Abdul Aziz kama mfalme mtarajiwa na kudumisha utulivu katika familia hiyo ya kifalme. Alijua kwamba kaka yake ni kibaraka wa Waamerika; hivyo basi, akabuni cheo cha mrithi wa kiti hicho cha ufalme ili kuhakikisha kuwa athari ya Uingereza, na akamteua kaka yake na kibaraka mwenzake, Muqrin bin Abdul Aziz, katika cheo hicho cha mrithi mwenza. Ili awe kibaraka wa Uingereza, kana kwamba aliona mbele kuwa Salman ni mkongwe na mgonjwa na hivyo basi kumpa fursa Muqrin kuchukua udhibiti hadi kifo cha Salman na kisha Muqrin kuchukua utawala kwa njia nyepesi. Kama ilivyo tokea wakati Fahad alipokuwa mzee na mgonjwa, na yeye, yaani Abdallah akawa wakati huo mfalme mtarajiwa na kuchukua udhibiti, na Fahad alipokufa mnamo 2005, Abdullah akachukua mamlaka. Lakini kilicho tokea baada ya kifo cha Abdallah mwanzoni mwa 2015 na kuchukua hatamu za uongozi kwa Salman haikuwa kwa hesabu za Abdullah; Salman alimtimua “Muqrin” kutoka kwa wadhifa wake na kumteua Muhammad bin Nayef kama mfalme mtarajiwa na mwanawe, Muhammad, kama naibu mfalme mtarajiwa, na kuwatimua wengi walioteuliwa na Abdullah katika nyadhifa nyeti, na kuanza kutilia nguvu mamlaka ya mwanawe, Muhammad, hadi mnamo 21/6/2017 alipomuondoa Muhammad bin Nayef kutoka kwa wadhifa wake na kumtangaza mwanawe kama mfalme mtarajiwa na kutomteua yeyote mwengine kuwa naibu mfalme mtarajiwa.

3- Tulitaja katika jibu la swali la mnamo 25/1/2015 baada ya Salma kuchukua mamlaka baada ya kifo cha Abdullah yafuatayo: mfalme aliyeko sasa, Salman, anatoka katika fani ya kijeshi, na hivyo basi, inatarajiwa kuwa athari ya Kiamerika imekita mizizi katika utawala wake, Abdullah alitambua hili, na kwa sababu hii alibuni ada mpya nchini Saudi Arabia, nayo ni, kuwa mfalme atateua sio tu mfalme mtarajiwa wake bali pia naibu mfalme mtarajiwa. Alitambua kuwa Salman bin Abdul Aziz anafuata Amerika, na kinyume na ada maarufu kuwa mfalme huteua mfalme mtarajiwa wake, mfalme Abdullah akateua naibu mfalme mtarajiwa kugawanya njia kati ya mfalme mpya, na kumteua mfalme mtarajiwa kutoka kwa vibaraka wa Amerika. Kwa hivyo, mfalme mwenda zake, Abdullah, alimteua kwa mapema naibu mfalme mtarajiwa; alimteua Muqrin kuwa mfalme mtarajiwa wa Salman bin Abdul Aziz kwa lengo tulilo tangulia kulitaja. Katika jibu la swali hilo, tulitaja: Muqrin anatambulika kwa mahusiano yake na Waingereza. Alisomea huko na kufuzu kutoka katika shule maarufu ya Cranwell nchini Uingereza. Aliaminiwa na mfalme mwenda zake Abdullah, na hata kuwa miongoni mwa washirika wake wa karibu. Ili kusitisha kuendelea kwa silsila ya vibaraka wa Amerika baada ya Salman bin Abdul Aziz, mfalme huyo mwenda zake akabuni wadhifa wa naibu mfalme mtarajiwa. Mfalme Abdullah aliidhinisha uteuzi huu kupitia kutoa azimio kuzuia kuondolewa kwa naibu mfalme mtarajiwa. Lakini hesabu za Waingereza zilikoseka kwa sababu Salman alikiuka mkataba huo pamoja na kanuni na ada, na kumuondoa Muqrin na kumteua kwa muda Muhammad bin Nayef na kisha kumtenga na kumfanya mwanawe, Muhammad, kuwa mfalme mtarajiwa na kumkabidhi mamlaka na nyadhifa kadhaa muhimu ili awe mtawala pekee.

*Endelea Uk..15*

4- Pindi baada ya mfalme Salman kutangaza kuunda kamati kuu ya kupambana na ufisadi mnamo 4/11/2017 chini ya uenyekiti wa mwanawe, Muhammad, mfalme mtarajiwa. Vikosi vya usalama viliwatia nguvuni Maamiri 11 na mawaziri 4 wa sasa na mara moja akawatimua afisini, ishara kuwa hili si jambo la kawaida na halina uhusiano na vita dhidi ya ufisadi, lakini ni sawia na yale yanayotokea katika mapinduzi, ambapo ukamataji hufanyika na utimuliwaji afisini na kushtakiwa hufanywa mara moja. Vile vile, ukamataji ulihusisha idadi kubwa ya mawaziri wa zamani na viongozi wa kibiashara na kufungiwa akaunti zao na akaunti za jamaa zao wa karibu, hii pia ikiwemo kufungiwa kwa zaidi ya akaunti 1700 za benki, ambapo haya "yanaongezeka kila saa" (Shirika la Reuters). Na miongoni mwa wale waliofungiwa akaunti zao ni akaunti ya Muhammad bin Nayef, aliye timuliwa wadhifa wake wa mfalme mtarajiwa hivi majuzi, pamoja na akaunti za idadi kadhaa ya jamaa zake wa karibu. Shirika hilo liliripoti, "Idara za Saudi zilisema zimewaweka kizuizini washukiwa zaidi, kwa sababu ya ukiukaji sheria, ambao ni watu wa familia ya kifalme na wafanyi biashara vilevile wakiwemo mameneja na maafisa kutoka ngazi za chini." Hili linathibitisha kuwa mchakato huu ni sawia na yale yanayofanyika katika mapinduzi. Kampeni hii ilipanuliwa kujumuisha watoto wa mfalme aliyetangulia; waziri wa ulinzi wa kitaifa, Meteb bin Abdullah (pia hutamkwa Miteb/ Mutaib), nguvu ya pili kuu sambamba na jeshi, na kakake Turki bin Abdullah, aliyekuwa Amiri wa Riyadh.

Na Metab bin Abdullah alifuzu kwa cheo cha luteni kutoka katika chuo cha mafunzo ya kijeshi cha kifalme cha Sandhurst ambacho ni chuo cha mafunzo cha jeshi la Uingereza ambapo kwa kawaida ni vibaraka wa Uingereza pekee ambao hupata mafunzo na kufuzu chuoni humo, naye alitanguliwa na wengi katika maamiri wa eneo la Ghuba na wafalme na maamiri wa Jordan. Kakake Turki bin Abdullah ana shahada ya uzamili (masters) katika sayansi na mikakati ya kijeshi kutoka chuo kikuu cha Uingereza cha Wales. Alifutwa kazi na Salman baada ya kuwa afisini kama Amiri wa Riyadh. Inaonekana kuwa Amerika imepata njia ya kuwango'a vibaraka wa Uingereza kupitia mashtaka ya ufisadi. Kwa hivyo, imemuagiza Salman na mwanawe, Muhammad, kutabanni njia ya kufanya hivyo, kama zifanyavyo serikali nyingi sasa kuwango'a wapinzani kwa kuwatuhumu kwa ufisadi. Hususan kwa kuwa watawala wote katika serikali hizi zilizo tangulia na zilizofuata zimechafuka kwa ufisadi, rushwa, wizi wa mali ya umma, mapendeleo kwa wale walio karibu yao na miradi inayo kiuka sheria, kuchukua haki za wengine, dhulma kwa raia na utumizi mbaya wa mamlaka yao kupata yale ambayo wao na washirika wao wanayo yataka. Na ni ufisadi upi mkubwa zaidi kushinda kuacha kufuata sheria za Allah na kufuata sheria za nchi za kikafiri za kikoloni?

5- Tumeona usaidizi wa Amerika katika kampeni hii na kwa wale wanaoitekeleza. Raisi wa Amerika kwenye ujumbe wake katika mtandao wa Twitter mnamo 6/11/2017, alisema: "Nina imani kubwa kwa Mfalme Salman na mfalme mtarajiwa wa Saudi Arabia, wanajua barabara kile wanachokifanya", akafuatiza na ujumbe mwengine: "Baadhi ya wale wanaokabiliana nao kwa ukali wamekuwa wakiikamua nchi yao kwa miaka mingi." Shirika la habari la Kisaudi lilisema kwamba "mfalme mnamo Jumapili 5/11/2017 alifanya maongezi ya simu na raisi wa Amerika katikati ya matukio haya ya kisiasa na kiusalama ndani ya Ufalme huo, na kujadiliana kuhusu ushirikiano baina ya nchi mbili hizi katika nyanja tofauti tofauti na njia za kuziboresha." Trump alizungumza na mfalme wa Saudia kuhusu kuiorodhesha kampuni ya Aramco katika soko la hisa la New York na kwamba angeshukuru endapo Riyadh itaorodhesha hisa za kampuni hiyo katika soko la ubadilishanaji la New York. Mfalme naye akajibu kwamba watafanya utafiti juu ya utumiaji wa soko la ubadilishanaji wa hisa la Amerika," Shirika la wanahabari wa kigeni la Reuters liliripoti haya mnamo 4/11/2017. "Tunaendelea kuzishajiisha idara za Saudia kuendelea kuwashtaki watu wanaoamini kuwa maafisa wafisadi; na tunatarajia kuwa watafanya hivyo kwa njia ya haki na uwazi," Msemaji wa wizara ya kigeni ya Amerika Heather Nauert alinukuliwa akisema haya na shirika la habari la Reuters mnamo 7/11/2017. Hii yaonyesha kuwa Amerika inasimama nyuma ya kampeni hii na kuiunga mkono na kuielekeza dhidi ya watu wasio takikana na Amerika au wale ambao inashuku utiifu wao kwa Amerika au ni vibaraka wa Uingereza au hawaridhishwi na yanayojiri na yale ambayo mfalme na mwanawe ambaye ni mfalme mtarajiwa wanayo yafanya ya kuiuza nchi kwa Waamerika kwa mwendo wa kasi.

6- Kinacho thibitisha kuwa kampeni hii ni kampeni halisi ya kisiasa ni kuwa kamati hiyo (ya kupambana na ufisadi) mara moja ilianza kazi yake ya kukamata na kufunga akaunti za watu muhimu serikalini, na watu wa familia hiyo ya kifalme na jamaa za mfalme…Hivyo basi, ni kampeni halisi ya kisiasa, na wala haina uhusiano wowote na ufisadi wala mageuzi, hususan kwa kuwa Salman na mwanawe wenyewe wamezama ndani ya ufisadi na ufujaji wa mali ya umma, ikiwemo ruzuku iliyopewa Amerika ya dola bilioni 460. Sauti ya taarifa iliyopeperushwa na shirika la habari la Saudia ilikuwa ya ukali kana kwamba ililenga kuzigonga nguvu zenye msemo zinazopinga serikali; ilielezwa katika taarifa hiyo, "Kuundwa kwa kamati hii ilitokana na kuwepo unyanyasaji unaofanywa na watu wenye nafsi dhaifu wanaoyapa kipaumbele maslahi yao binafsi juu ya maslahi ya umma, na kuiba pesa za umma pasi na kupata kizuizi cha kinafsiya kutoka katika dini, akhlaqi au utaifa. Wakitumia fursa ya athari waliyo nayo na mamlaka waliyo kabidhiwa katika kufuja na kubadhirisha pesa, huku wakitumia

*Endelea Uk..16*

njia kadha wa kadha kuficha vitendo vyao hivi vya kufedhehesha. Na kisha ukamataji huu ukakolezwa mara moja baada ya kuundwa kwa kamati hii mnamo 4/11/2017.

7- Kisha baada ya hapo mnamo 5/11/2017, ilitangaza kuwa Naibu wa Gavana wa eneo la Asir, Mansur bin Muqrin, pamoja na baadhi ya maafisa waliuwawa katika ajali ya ndege aina ya helikopta, na kuna shaka kuwa tukio hili linahusiana na ung'oaji huu. Hususan kwa kuwa amiri huyu ni mtoto wa Muqrin, aliyekuwa mfalme mtarajiwa aliye timuliwa na Salman baada ya Salman kuchukua mamlaka moja kwa moja. Idadi ya walio kizuizini imezidi mamia. Sa'ud Al-Mu'jab, mkuu wa sheria wa Saudia, alisema: "Watu 208 wameombwa wafike kuhojiwa kuhusiana na uchunguzi wa ufisadi, saba kati yao wameachiliwa huru kwa kukosekana ushahidi wa kutosha… Thamani ya kipesa ya matendo haya ya miongo mingi yamehusisha viwango vikubwa vya pesa zilizo badhirishwa na kufujwa na thamani ya kihakika ya viwango hivi huenda ikazidi dola bilioni 100 za Kiamerika kulingana na yale yaliyojitokeza katika uchunguzi wa mwanzo" (Al-Hayat, 9/11/2017). Upekuzi huu umekuwa ukifanywa kwa miongo kadhaa ndani ya stakabadhi za jamaa wa familia ya kifalme na wenye msemo katika utawala, inayo ashiria kuwa kadhia hii ni ung'oaji tu wa watu mamlakani na athari katika utawala ambao huenda ukageuza mambo kwa mfalme mtarajiwa mwana wa Salman endapo hatatekeleza ung'oaji huu maalum ili kuleta mabadiliko yasiyo ya kawaida kwa serikali na kwa jamii nchini humo, juu ya kuwa amepanda ngazi ya kuwa mfalme mtarajiwa wakati hastahiki kuchukua wadhifa huo kuambatana na ada za familia hiyo…

8- Hivyo basi, yanayo endelea nchini Saudi Arabia chini ya kinachoitwa kampeni dhidi ya ufisadi ni kuwakata Waingereza na kuwazuia kupanga njama ya jaribio la mapinduzi au, pengine, dhidi ya Mfalme Salman na mwanawe mfalme mtarajiwa, pamoja na kufaulisha ugurishaji salama wa utawala kwenda kwa mfalme mtarajiwa ili asiwepo yeyote wa kumpinga; kwa kuwa mwana huyu amejitolea kibinafsi kutumikia maslahi ya Amerika pasi na kuwepo utesi wa kindani hata kama ni kwa jamaa yake wa karibu! Na kutoka kwa wapinzani wote wa kinje, hususan Uingereza, ili kudumisha athari iwe pekee kwa Amerika kisiwani humo… Hivyo basi, uhaini huu haugawanyiki

(وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي كَيْدَ الْخَائِنِينَ)
"… na kwamba Allah haziongoi hila za makhaini" [Yusuf: 52].

9- Mwisho, kila siku inapopita inathibitika kuwa hakuna kheri ndani ya serikali zote hizi: si kwa serikali ya familia ya Saud wala serikali ya Iran wala kwa serikali yoyote iliyoko katika biladi za Kiislamu wala kwa wale wanaowafuata na kutii maamrisho yao. Zinaendeshwa na makafiri wakoloni wanaofanya kazi kuendeleza ukoloni wao juu yetu na kufuja utajiri wetu kwa uongozi huo. Hivyo basi, hakuna budi kipaumbele cha mwanzo katika kazi kiwe ni kubadilisha sura halali ya serikali hizi, zilizo egemea matakwa ya kafiri mkoloni.

(وَلَا تَرْكَنُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ ثُمَّ لَا تُنْصَرُونَ)
"Wala musiwategemee wale wanaodhulumu, usije ukakuguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Allah, wala tena hamtasaidiwa" [Hud: 113].

Kisha kuondoa muozo wote huu na ufisadi uliosababishwa na nchi za kikoloni, ima Amerika au Uingereza au nyenginezo, kwani ukafiri ni mila moja katika uadui wake dhidi ya Uislamu na Waislamu… Na wote wanaofuata nchi hizi au wanaoshirikiana nao kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja na kutabikisha mipango yao na miradi yao na kudumisha nidhamu zao za kisekula ni wahalifu na wataadhibiwa kwa fedheha.

(سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ)
"Itawafikia hao walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Allah kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya." [Al-An'am: 124].

Suluhisho hili la matatizo yetu na wala hakuna suluhisho jengine: ni kung'olewa kwa serikali hizi na kuasisiwa Khilafah Rashidah katika njia ya Utume… hata kama litakataliwa na wenye shaka na kuonekana kama jambo gumu na walegevu, lakini ikhlasi kwa Allah (swt) katika kazi hii na ukweli katika kumuiga Mtume (saw) italifanya jambo lililo mbali kuja karibuni kwa idhini Yake (swt),
وَيَقُولُونَ مَتَى هُوَ قُلْ عَسَى أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا
"Watakutikisia vichwa vyao, na watasema: Lini hayo? Sema: A'saa yakawa karibu!" [Al-Isra': 51]

Hapo ndipo ahadi ya Allah itakapotimia.
وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ
"Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusra ya Allah, humnusuru amtakaye Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu" [Ar-Rum: 4-5]

**2 Rabii' I 1439 H**
**20/11/2017 M**


Email: uqab@hizb.or.ke